**MTIHANI WA PAMOJA WA KASSU**

Hati ya kuhitimu kisomo cha secondary

102/3

KISWAHILI Karatasi ya 3

**MWONGOZO**

FASIHI

SEPTEMBA 2021

(SIRI)

**1.USHAIRI**

Kama Sodoma!

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Haitaji makini, kwa mwenye macho mazima
Utaona walkini, mradi ukitizama
Wanazini hadharani, wana kwa watu wazima
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Wanazini hadharani, wana kwa watu wazima
Wanafatuna maini, vijana na kina mama
Hawana haya nyusoni, wameharamisha wema
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini,kidogo kama Sodoma!
Hawana haya nyusoni, wameharamisha wema
Baba na binti ndani, wanacheza lelemama
Marijali wa mbioni, kujipagaza umama

Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Marijali wa mbioni, kujipagaza umama
Wameikataa dini, toka tumboni mwa mama
Wadai Wataliani, watajirisha mapema
Yafanana na sodoma, mji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Wadai ufirauni, watajirisha mapema
Hivyo mabo ya kigeni, yametunukiwa dhima
Uwaonapo fuoni, nusu uchi wa mnyama
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Uwaonapo fuoni, nusu uchi wa mnyama
Watu hawana imani, umezidi uhasama
Watu hawana imani, umezidi uhasama
Na viongozi wa dini, kuabudu darahima
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama sodoma!
Na viongoai wa dini, kuabudu darahima
Wamekeuka yamini, kati yao na Rahima
Wamemuasi Manani, na kusahau kiyama
Yafanana na sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Wamemuasi manani, na kusahau kiyama
Ya Illahi tuauni, tuwe watu maamuma
Tukue katika dini, siku zetu za uzima

Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

**Maswali**

(a) Bainisha bahari ya shairi hili ukijikita katika ruwaza zifuatazo (alama3)

(i) Mishororo

-Takhmisa –mishororo tano

(ii) Maneno

- Pindu-utao, mshororo wa mwisho wa ubeti unafanywa ukwapa wa mshororo wa kwanza ubeti unaofuata
- Kikwamba – Neno/ukwapi wa mshororo wa kwanza kila ubeti ni lile/yale yale

(ii) Vina – mtiririko

- Vina vyote, vya ndani vina urari (ni) aidha vina vya nche vina urari (ma)

(b) Eleza muundo wa shairi hili (alama4)

- Beti nane
- Mishororo 5 kila ubeti
- Bipande viwili kila mshororo
- Mizani kumi na sita kila mshororo
- Vina vya ukwapi ni ‘ni’ na vya utao ni ‘ma’
- Lina kibwagizo
-

(c) Bainisha mbinu zifuatazo za kimtindo katika shairi hili (alama3)

(i) Tashbihi –kidogo kama Sodom!

(ii) Taswira-uwaonapo fuoni, nusu uchi wa mnyama

Tasfida-wanatafuna maini (kushiriki ngano)

(d) Eleza toni ya shairi hili (alama1)

- Kukashifu/kusuta/kushauri

(e) Bainisha nafsi nenewa katika shairi hili (alama1)

- Wanajamii

(f) Fafanua dhamira ya mtunzi wa shairi hili (alama2)

- Kukashifu utovu wa maadili katika jamii/mijini
- Kuonyesha uozo uliopo mijini

(g) Andika ubeti watatu kwa lugha tutumbi (alama4)

- Hakika, miji yetu imekuwa kama Sodoma.
- Watu hawana haya kwani wametupilia mbali maadhili
- Baba na binti zao hishiriki mapenzi wasichana wadog kuwa waja wazito. Miji yetu inafanana na Sodoma.

(h) Fafanua maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa na mshairi (alama2)

- Manani – Mola/Mungu
- Marijali-wasichana /mabiti

**2.RIWAYA YA CHOZI LA HERI.**

(a)(Madhila anuwai yanayowazonga wahusika wengi katika riwaya ya Chozi La Heri yanafungamanishwa na hiari ya maamuzi yao. Jadili (al.20)

Wahusika katika riwaya ya Chozi la Heri wanakumbwa na matatizo mbalimbali. matatizo hayo ni ya kiuchumi na kijamii. Vyanzo vya matatizo yenyewe ni tofauti tofauti, kuna yale yanasababishwa na wahusika wenyewe ilhali mengine yanaletwa na watu wengine. Tunaweza kusema kuwa matatizo mengine yanatokana na uamuzi mbaya wanaaoufanya wahusika wenyewe.

- Jumba moja la Ridhaa linabomolewa kwa kuwa alilijenga katika ardhi iliyotengewa ujenzi wa barabara katika mtaa wa zari. Hakuchunguza uhalali.

- Terry mkewe Ridhaa anapuuza maonyo na maneno ya mumewe kuhusu mkasa ambao ungetokea hivyo anateketea.

- Ami wa Mwamwangeka anaagamia katika mkasa wa moto alipoenda kuwasaidia watu waliokuwa wanateketea.

- Walioteketea katika moto wa lori walijiigiza matatani wenyewe kwani walikuwa wameonywa kulikuwa na hatari.

- Uhasama, migogoro na ukosefu wa mahitaji muhimu unaoikumba familia ya Mwimo Msubili hii ni kwa sababu ya yeye kuwaoa wake wengi.

- Kufutwa kazi kwa Lunga Kangata Kiriri baada ya kukataa kukubali mahindi ya jano kuuziwa wananchi ni tokeo la uamuzi na msimamo wake..

- Mauti yanayowakumba vijana waliokuwa wakiandamana baada ya sherehe za kuapishwa kwa kiongozi mpya.

- Tendo la Subira kuondoka nyumbani na kumwacha mumewe linaisambaratisha familia yake na hatimaye kuletea maangamizi mwenyewe.

Pete anapokubali kuolewa na Nyangumi bila kufanya uchunguzi wa kina ni uamuzi uanokuja kumvnja moyo baadaye baada ya mke halisi wa Nyangumi kurudi.

- Tukio la Zohari kupata mimba na kutumbukia katika mateso mengi linasababishwa na uamuzi wake wa kushiriki katika mapenzi akiwa shuleni kidato cha pili.

- Tendo la Mwangeka na Mwangemi kufanyia babu yao mzaha, kwa kuwa usiku mmoja aliamua kuwalipua viboko.

- Mwangeka anakubaliana na Tila kuigiza maombolezi ya Dedan Kimathi ambayo yanamfanya babake kumwadhibu kwa kutowajibika.

- Kukamatwa kwa Sauna na mwajiri wake Bi. Kangara kwa kujihusisha na Biashara ya ulanguzi wa watoto.

- Tuama anaathirika vibaya baada ya kupaswa tohara na kulazwa hospitalini ni tendo alilolitenda kinyume na mapenzi ya baba yake.

- Walevi wenza wa Shamsi ambao wanapoteza uwezo wa kuona au uhai wao kwa kubugia vileo.

- Mumwewe Selume anamfukuza mkewe kwa kuwa si wa kabila lake baadaye anamlea mtoto Sara peke yake.

- Mandu anapouawa katika vita akiwa ughaibuni ni hiari yake kwani huenda hangepoteza maisha kama hangeenda huko mapema.

- Fujo zinazosababishwa na wahafidhina baada ya uchaguzi ambapo wanapoteza uhai na mali.

- Wakimbizi waliohamia katika msitu na kupanda mimea na baadaye kufukuzwa ilikuwa ni hiari yao kwani si halali kulima msituni.

- Naomi kumwacha mumewe Lunga Kiriri na watoto na baadaye kuwatafuta baadhi ya kifo cha
- bwanake Zozote **(20 x 1) = 20)**

(b) "Nakumbuka asubuhi ya pili baada ya mtafaruku kuanza. Nilikuwa sebuleni na wanangu tukitazama runinga. (uk.20)

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama4)**

Msemaji ni Kaizari

Msemewa ni Ridhaa

Walikuwa katika kambi la wakimbizi.

Kaizari alimsimulia Ridhaa kadhia zilizotokea baada ya uchaguzi

**4 x 1 = 4**

(ii) Eleza nafasi ya msemaji katika kuwakuza wahusika wengine riwayani. **(alama5)**

Msemaji ni Kaizari

i. Ametumika kuonyesha jinsi ukimbizi ulivyovunja hadhi ya aliyekuwa <u>Waziri wa Fedha</u>. Anaonekana aking'ang'ania chakula na wakimbizi wengine.
ii. Anawasilisha matatizo yanayowakumba <u>Lime na Mwanaheri</u> kambini. Wao wanapigwa na matone ya mvua kwa kukosa makazi.
iii. Anaonyesha mabadiliko ya kiwajihi yaliyomkumba <u>Subira</u> baada ya kuvamiwa. uk. 16
iv. Ametumiwa kubainisha malalamishi ya <u>Tetei</u> kuhusu ubaguzi unaoendelezwa dhidi ya wanaume.
v. Ametumiwa kubainisha bidii za Mwekevu. Mwekevu alijitosa kwenye uga wa siasa na kuomba kura kama walivyofanya wanaume.
vi. Ametumiwa kuonyesha ukatili wa kijana aliyevalia shati lililoandikwa '<u>Hitman</u>'. Analirushia bomu la petrol gari lililokuwa likipinduka kana kwamba alikuwa akinyunyizia viwavi dawa.
vii. Anaonesha utu wa mhusika <u>Tulia</u>. Tulia alienda kwa nyumba ya Kaizari ili kuwaokoa wakati wa uvamizi.
viii. Ametumia kuonyesha umaskini uliomkumba <u>Makiwa</u> na wenzake katika Mtaa wa Sombera.
ix. Ametumiwa kusawiri tabia ya ufisadi ya <u>Bwana Kute</u>. Bwana Kute anatumia ujanja ili kupata mafungu zaidi ya vyakula vya msaada.

**zozote 5 x 1 = 5**

(c) (i) Tambua mtindo uliotumika katika dondoo hili. **(alama1)**

Mbinu rejeshi: Msimulizi anasimulia matukio yaliyotukia awali. 1 x 1 = 1

(ii) Eleza jinsi mbinu uliyotaja katika (c) (i) ilivyotumika kukuza maudhui riwayani.

**(alama10)**

(iii)Kupitia mbinu rejeshi maudhui yafuatayo yanakuzwa:

i. Ushirikina – Ridhaa anakumbuka matukio kama vile: kupepesa kwa jicho lake la kulia kwa muda wa wiki mbili mtawalia, kuanguka kwake bila kuona kilichomkwaa na jeshi la kunguru lililotua katika paa la maktaba yake. Aidha, anakumbuka milio ya kereng'ende na bundi usiku. Matukio hayo yote ni ishara ya mambo mabaya ambayo yangetokea.
ii. Ubabedume – Ridhaa anakumbuka maneno ya marehemu mama yake kuwa unyonge haukutunukiwa majimbi bali makoo (uk. 3).
iii. Usaliti – Kedi, ambaye alikuwa jirani ya Ridhaa, anamsaliti Ridhaa kwa kuteketeza jumba lake pamoja na jamaa zake.
iv. Uharibifu wa mali – jumba la Ridhaa linateketezwa. Aidha, mahindi katika shamba la Ridhaa yanateketezwa.
v. Mauaji/ukatili – Terry, Lily Nyamvula, Annatila na Becky wanauawa baada ya nyumba yao kuchomwa moto.
vi. Vita – Mwangeka alikuwa ameenda kudumisha amani katika Mashariki ya Kati.
vii. Ukoloni mamboleo – Hata baada ya uhuru, mmiliki wa mashamba ya Theluji Nyeusi ni mlowezi maarufu. Aidha, Myunani anayamiliki maekari na maekari ya mashamba katika eneo la Kisiwa Bora ambapo wenyeji wamegeuzwa kuwa maskwota.
viii. Utegemezi – Kwa mujibu wa Tila, wenyeji hawana mashamba wanategemea wageni kwa vyakula na ajira.
ix. Udhalimu – sheria za kikoloni zilimpa Mzungu kibali cha kumiliki mashamba katika sehemu zilizotoa mazao mengi. Hali hii iliwalazimu Waafrika kama Msubili kuwa maskwota au vibarua katika mashamba ya wakoloni.
x. Utumwa – vijulanga vilinyakuliwa kutoka kwenye susu zao, hata vifua havijapanuka; na kupelekwa katika maeneo mbalimbali kufanya kazi.
xi. Upangaji uzazi – Mwimo Msubili alikuwa na watoto wa kiume ishirini. Hivyo, ardhi iligawanywa hadi haingewatosha tena. Aidha, Msubili anakabiliwa na changamoto ya kuwalisha wanawe wengi.
xii. Mgogoro katika familia – Wingi wa vinywa vya kulishwa katika familia ya Msubili ulizua mgogoro, uhasama na uhitaji mkubwa.
xiii. Ubaguzi – Ridhaa anatengwa na wanafunzi wenzake kwa kuwa walimwona kama Mfuata Mvua.Hawakumchukulia kuwa, alikuwa mmoja wao.
xiv. Elimu – Mamake Ridhaa anatilia mkazo umuhimu wa elimu. Anadai kuwa, elimu inapaswa kuwa chombo cha kueneza amani na upendo.

xv. Uhasama wa kisiasa unasababisha kuvunjika kwa ujirani – Kedi ndiye aliyemtafutia Ridhaa shamba alilolijenga. Aidha, Ridhaa alidhamini masomo ya wapwa wake wawili. Hata hivyo, Kedi anashiriki katika mauaji ya jamaa za Ridhaa.

xvi. Vitisho – vikaratasi vilisambazwa kuwatahadharisha akina Ridhaa kuwa, kuna gharika baada ya kutawazwa kwa Musumbi (kiongozi) mpya.

xvii. Unyakuzi wa ardhi – baadhi ya mabwanyenye wanajenga majumba mahali ambapo pametengwa kwa ajili ya upanuzi wa barabara. Mengine yalijengwa chini ya vigingi vya nyaya za stima.

xviii. Ufisadi – kuna mabwanyenye ambao wanaonekana wakitoa milungula hadharani.

xix. Ndoa- kwamba si wanawake pekee watesekao katika ndoa. Kuna wanaume ambao wanateseka kutokana na mapigo na dhuluma za kisaikolojia kutoka kwa wake zao (uk. 17).

xx. Mabadiliko – wimbi la mabadiliko liliwakumba Wahifidhina kisiasa ambapo mwanamke anachaguliwa kama kiongozi kinyume na ilivyokuwa hapo awali.

xxi. Umuhimu wa vyombo vya dola – vyombo vya dola vilitumwa ili kudumisha usalama katika vijiji na mitaa.

xxii. Wizi – wengine waliingia katika maduka ya Kihindi, Kiarabu na hata ya Kiafrika na kupora walichoweza kubeba.

xxiii. Sheria – Kaizari anadai kuwa waporaji walikibeba walichoweza kukibeba kabla ya kukutana na mkono mrefu wa utawala.

xxiv. Utamaduni - kupitia mbinu rejeshi, mwandishi anasimulia kuhusu mitindo ya mazishi katika jamii ya akina Ridhaa. Mwangeka anakumbuka jinsi watu walivyoomboleza kifo cha nduguye, Dede

xxv. Ubakaji – Sauna alibakwa na babake mlezi, Bwana Maya.

**zozote 10 x 1 = 10**

**3 Tamthikia ya KIGOGO.**

.(a) (i) “Ama kweli dunia gunia . Ilikumeza hindi bichi ikakuguguna, sasa inakutema guguta.”

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. **(alama4)**

Msemaji ni Majoka

Msemewa ni Ashua

Walikuwa katika ofisi ya Majoka.

Majoka alikuwa akimdhihaki Ashua kutokana na matatizo aliyopata kwa kutompenda.

**4 x 1 = 4**

(ii) Eleza mbinu mbili za kimtindo katika dondoo. **(alama2)**

(i) Taswira: sasa inakutema guguta; dunia gunia

(ii) Tashihisi: Dunia inapewa sifa ya kumeza.

(iii) Kejeli/dhihika: Majoka anamdhihaki Ashua kwa kutompenda na kuishia kumpenda Sudi aliyemletea tabu tu.

**zozote 2 x 1 = 2**

(iii) Masaibu yanayowakumba wahusika katika Kigogo ni zao la matendo yao ya awali. Fafanua kauli hii kwa kutolea mifano mwafaka tamthiliani. **(alama12)**

(i) Majoka anamuua Jabali kupitia ajali. Tunu anataka kuwaleta wachunguzi wa nje ili kuchunguza ajali hiyo, hali inayomtia wasiwasi.
(ii) Majoka analifunga soko la Chapakazi, hali inayowachochea raia kuandamana na kumng'atua mamalakani.
(iii) Ngao Junior anatumia mihadarati, hatimaye inamuua kwenye uwanja wa ndege.
(iv) Majoka anawaruhusu wanafunzi katika shule yake kudungana dawa za kulevya, hivyo kuwasababisha wote kuanguka mtihani.
(v) Boza anamruhusu Ngurumo kuuza pombe na mkewe Mamapima, hatimaye Ngurumo anajihusisha kimapenzi naye.
(vi) Ngurumo anaunga mkono uongozi wa Majoka lakini uongozi huo unakuja kumuua hatimaye. Anauliwa na kundi la watu analolitumia Majoka kuwaua wapinzani wake.
(vii) Hali ya mumewe Bi. Hashima kutokuwa na bima karibu iifanye familia yake ikose fidia kutoka kwa Majoka alipokufa akifanya kazi katika kampuni yake.
(viii) Majoka ana kampuni kubwa zaidi inayozalisha dawa za kulevya ambazo zinakuja kumuua mwanawe, Ngao Junior.
(ix) Kitendo cha Husda kutokuwa na mapenzi ya dhati kwa mumewe Majoka kinamfanya kuaibishwa na Majoka hadharani anapomwambia hadharani kwamba hampendi.
(x) Majoka anamfungulia biashara ya kukata miti, hali inayotishia mvua kutonyesha jimboni, hivyo kuathiri maisha ya raia.
(xi) Majoka anampa Mamapima kibali cha kuuza pombe haramu ambayo hatimaye inawaua na kuwapofusha raia.
(xii) Majoka anawaua raia wengi, hali inayomsababisha kujiona akiwa amefungwa mikono kwa monyororo ndani ya ziwa la damu anapozirai.
(xiii) Chopi anakubali kutumiwa na Majoka kuwaua wapinzani wake kama Tunu lakini naye anapokosa kumuua Tunu alivyoagizwa, Majoka anaanza kupanga mauaji yake.
(xiv) Kombe anaunga mkono mrengo wa majoka unaowadhulumu raia badala ya kuupinga. Majoka anaanza kusambaza vijikaratasi vinavyolitaka kabila lake Kombe kuhama Sagamoyo kwa madai kuwa si kwao.
(xv) Wafanyabiashara kama vile Kombe na Boza walihamia ulevini Majoka alipofunga soko badala ya kushirikiana na raia wengine katika maandamano ili kuupinga udhalimu huo, hali inayomsababisha Majoka kudinda kulifunga soko.

**zozote 12 x 1 = 1**

(b) Ubinafsi una athari mkubwa katika jamii.Tetea kauli hii ukitolea hoja ishirini kamilifu katika tamthilia ya kigogo. **(alama20)**

- ✔ Umaskini-unyakuzi wa soko la chapakazi inafanya wasagamoyo kushindwa kukimu mahitaji yao.mfano ashua kuwa ombaomba.
- ✔ Ari ya mapinduzi –tamaa na ubinafsi wa watawala vinawakasirisha wenzake.Tunu na sudi kuanzisha harakati za kuungoa mamlakani uogozi wa majoka.
- ✔ Uchafu wa mazingira-tamaa ya wanaviwanda inasukuma kutupa kemikali kwenye mitaro ya maji hivyo kusababbisha uchafuzi wa mazigira.
- ✔ Utabaka- kutokana na tama ya majoka ya kutaka kumiliki mali anaendeeleza ukiritimba kwa sababu ya kumiliki makampuni ,shule za kifahari na maeneo ya kujiburidisha ilhali kuna wenye ni maskini mfano wale walevi mangweni.
- ✔ Matumizi mabaya ya vyombo ya dola-kutokana na tama kutaka kusalia mamlakani majoka natumia vyombo vya dola vibaya .k.m majoka anatumia kwa mfano polisi kutekeleza unyama ,wachuuzi watano kuuawa kwa sababu ya kuuandamana.
- ✔ Ukame-Hashima anaeleza kuwa msimu wa kulima mchele ulikuwa mbaya .Maziwa ma mito imekauka kwasababu ya majoka kuudhinisha ukataji miti.
- ✔ kuathirika kisaikolojia-Tamaa na ubinafsi wa majoka unamfanya kutekeleza ukatili ambao unaifanya nafsi yake kumhukumu nkupitia mazungumzo yake na babu .
- ✔ Unyanyasaji-tamaa na ubinafsi wa viongozi vinawasukuma kukusanya kodi kubwa na hata kushirki ufisadi kutoka kwa wachuu-
- ✔ Tamaa ya kumiliki hoteli inamfanya majoka kuwapokonya raia ardhi ya soko lao ili kujenga hoteli yake
- ✔ Tamaa ya pesa inamsababishia Ngurumo kutotaka soko lifunguliwe .Anasema kuwa tangu soko lifungwe mauzo ya pombe yalikuwa maradufu.
- ✔ Tamaa ya pesa inamsababisha mama pima kuwakipia raia ppombe haramu bila kuwazia madhara iliyowasababishia-kifo na upofu.
- ✔ tamaa inamsababishia Ashua kutoridhika na kile alichokuwa nacho mumewe .Anataka zaidi ya uwezo wa mumewe.
- ✔ Tamaa ya kutaka familia ya ngao kusalia mamlakani daima inasababisha majoka kutaka kumridhisha mwanawe ngao junior uongo wa sagamoyo.
- ✔ Tamaa ya pombe inawanya wafanyabiashara kuenda kulewa badala ya kuungana na wenzake katika kupigania kufunguliwa kwa soko la chapakazi.
- ✔ Tamaa ya kutaka kupata kadarasi ya kuoka keki inamfanya Asiya kumoa Ngurumo uroda ili apawe kandarasi yenyewe.
- ✔ Tamaa ya uongozi inamsababishai majoka kumuua Jabali koongozi wa chama cha mwenge kwa kuwa hataki mpinzani.
- ✔ Tamaa ya mali inamsabishia Husda kukubalia kuolewa na Makoka licha kuwa hakumpenda.uk 75
- ✔ Tamaa ya pesa inamsababishia mkurugenzi katika kampuni ya majoka kupandisha bei ya chakula kwenye kioski cha kampuni mara dufu.

- ✔ Tamaa ya kimwili inamfanya majoka kumtamani Ashua ilhali ana mke Husda.Vilvile alitaka kumrithi X baada ya mumewe kuaga.
- ✔ Tamaa ya utajiri unamsababishia Kenga kukubali kutengewa kipande cha ardhi ya soko la chapakazi ambayo ilikuwa ardhi ya umaa.

**(20x1)**

**4 TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE**

(a) " Fujo hazitatuhamisha hapa panapo ardhi yetu. Kwa kurejelea kauli hii jadili namna ambavyo wanyonge katika hadithi ya Tumbo Lisiloshiba walivyojiopoa kutoka kwa dhulma za uongozi mbaya (alama8)

i. Mzee na Mago na wenzake walijikaza ili kuzia njama za watu wakubwa kutaka kuchukua ardhi za watu na kuharibu maisha yao.
ii. Mzee Mago aliwahamasisha wenzake kuhusu Mzee Mago unyang'anyi wa Uraia
iii. Kuwaambia umuhimu wa kuishi kwa amani na furaha popote pale nchini mwao
iv. Wanashauriana namna ya kureruka vitego na vikwazo vya sharia vinavyowekwa makusudi ili wao wtu wadogo wasiweze kutetea mali yao.
v. Wanafafuta wanasheria waaminifu ili kutatua mazonge ya sharia ngumu zilizowakabili
vi. Wanataka kushirikishwa katika maendeleo yanayopiga kasi nchini mwao.
vii. Viband vyao vinapobomolewa vinajengwa upya

(b) Kwa kurejelea hadithi zifuatazo, jadili nafasi ya Elimu katika Jamii (alama12)

i. Mapenzi Kifaurongo
ii. Shogake dada ana ndevu
iii. Mame Bakari

**Mapenzi Kifaurongo**

- Masomo kuwalemea wanafunzi mfanoDenis Darasani haelewi chochote.
- Wahadhiri anawafisha moyo wanafunsi mfano Daktari mabonga.
- Shule za mikoa/za kitaifa huibuka mabingwa katika masomo.
- Elimu ni ghali- Denis amesoma kwa taabu
- Elimu haipeani nafasi ya kazi-mfano Deniss (kadiria)

**Shogake dada and ndevu**

- Mtihani ndio daraja ya kuwafusha wanafunzi kuelekea hatua nyingine mfano-Safia anasubiri kufanya mtihani utakaomuusha.
- Wanafunzi wanakosa maadili kwani wandanganya wanafunzi kuwa wanadurusu ilhali wanazini
- Kila mwanfunzi ananuia kuwa wa kwanz katika masomo kwa mfano Safia kuibuka wa kwanza katika darasa lake.

**Mame Bakari**

- Wanfunzi husoma masomo ya ziada wakati wa usiku mfano Sara anabakwa akitoka shuleni usiku
- Elimu ina jukumu la kuwaadilish a wanafunsi, Sara anakataa wazo la kuiavya mimba yake kwa sababu ya shairi la usiniuwe
- Mimba huathiri elimu ya wanafunzi . Sara anauna kuwa angefukuzwa kutoka shuleni iwapo mwalimu mkuu angejua kuwa yeye ni mjamzito.

(b) Looh! Kwani swali langu liko vipi? Kwa nini wanafunzi wanacheka? Dkt. Mabonga hacheki safari hii kwa nguvu. Haikosi nimemuudhi.

> " Hilo si swali," anasema. "Iwapo ulinuia kuchekesha ungenyamaza tu. Hatukuja hapa kuchekeshwa. Tena pale ulipo hujui kuchekesha."

**i)** Bainisha mbinu za kimtindo zilizotumiwa kwenye dondoo hili. **(alama6)**

ii) "Hadi sasa mimi ni kama rubani aliyeharibikiwa na ndege angani."
Eleza maana ya kitamathali inayojitokeza kwenye kwenye dondoo hili. **(alama14)**

( i)

- Siyahi/nidaa- Looh!- kuonyesha mshangao
- Balagha- kwa nini wanafunzi wanacheka?
- Kejeli- Tena pale ulipo hujui kuchekesha
- Nahau- kuufyata ulimi- kunyamaza
- Jazanda- 'nikizimwa'- nikinyamazishwa/nikidhalilishwa/nikidhulumiwa
(6x1= 6)

(ii)

- Kukosa utulivu darasani- Dennis anasema , "Nimo darasani lakini hakuna niachokipata. Akilini mawazo yamenitatiza" (uk. 12)
- Dennis kuishi kimaskini- anatamani mavazi mazuri ya wenzake pale chuoni.
- Dennis pamoja na wenzake hawaelewi kile ambacho Dkt. Mabonga anafundisha (uk. 14)
- Dennis anapomwomba Dkt. Mabonga atumie lugha nyepesi, wenzake wanamcheka huku akikejeliwa na Dkt. Mabonga. (uk.15)
- Dennis anawasikiliza wanafunzi wenzake wanavyojigamba na kujishaua wakiacha masoma wana nafasi za ajira au usaidizi wa kifedha. Anapojilinganisha nao, fikira hizo zinamsakama na kumziba kauli. (uk. 16)
- Dennis hana vitu vya thamani chumbani mwake- shuka za kitanda chake zimezeeka na kuchanika.

- Dennis kukosa chakula. Hana mchele wa kupika chamcha. Analazimika kupika uji mweupe usio na sukari. (k. 17)
- Dennis anaingiwa na aibu na wasiwasi wakati msichana mrembo anapobisha hodi na kujitoma chumbani mwake. Anaaibika anapomuuliza mbona anakunywa uji majira hayo. (uk. 19)
- Penina anapomtaka Dennis kimapenzi, Dennis anayatia maneno yake katika mizani na kujiuliza maswali mengi kuhusu kauli zake. Haamini binti wa kitajiri anaweza kumpenda yeye kijana wa kimaskini. (uk. 21)
- Baada ya kufuzu chuoni, ilikuwa vigumu kwa Dennis kupata kazi. Anasema, " kupata kazi ni vigumu. Kazi iliyobaki nchini nikutafuta kazi." (uk. 22)
- Dennis alipoalikwa kwenye mahojiano ya kazi ya uanahabari, anakutana na Shakila binti mmoja waliyesoma naye chuoni. Shakila aliwahi kujinaki kuwa mamake ni mkurugenzi wa shirika la uchapishaji wa magazeti nchini. Dennis anaona itakuwa muhali kwake kuipata kazi ile pale. (uk. 23)
- Dennis anashindwa kujibu maswali kwenye mahojiano na anafukuzwa na mwamamke mkuu wa mahojiano hayo kwa kejeli.
- Dennis anapokosa kupata ajira, Penina anamdharau na kusema yeye ni bwege-hampi chakula wala maji. (uk. 28)
- Penina anamfukuza Dennis kutoka kwa nyumba yake na kumweleza nyumba hiyo aione paa. (uk. 27)
- Dennis anapokosa kazi anatambua mapenzi ya kifaurongo ya Penina. Anasema ameachwa mchege hana kazi hana bazi. (uk.28)
- Dennis anawawazia wazazi wake wanaokula mwata nyumbani. Anaiona elimu aliyoisoma haileti matumaini. (uk. 28)
- Dennis ana wasiwasi kuhusu kesho yake. Anasema akijaliwa kumpata mke atakayemkubali na umaskini wake au akimkosa atashukuru tu. (uk. 28) (14x1=14)

**5 FASIHI SIMULIZI**

5.a Eleza maana **ya semi katika fasihi simulizi** **(alama 2)**

a) **Semi**

- Ni kauli fupi za kisanaa zenye maana na mafunzo yaliyofichika.
- Semi ni tungo za fasihi simulizi ambazo ni fupifupi ;zenye kutumia picha, tamathali na ishara

b) Sifa za semi

- Huwa fupi kwa kuwasilisha ujumbe mrefu kwa maneno machache.
- Maana hupatikana katika jamii iliyozibuni.
- Ni tanzu tegemezi kwa hutegemea tanzu nyingine kama vile hadithi, mazungumzo, n.k.
- Hazibadiliki vivi hivi.
- Hufumba ujumbe wake.
- Baadhi ni kielelezo cha maadili k.v. methali
- Hutumia lugha ya kimafumbo
- Huibua taswira
- Huwa na mchezo wa maneno
- Baadhi huwa na muundo maalum k.v. methali na vitendawili
- Baadhi zikikosa kutumika hutoweka k.v. misimu

**Zozote sita**

c) Mambo ya kuzingatia ili kufanikisha uigizaji jukwaani

- Nitakuwa mchangamfu na mcheshi kwa hadhira ili kuwafanya wapendezwe na maigizo.
- Nitahakikisha nimeufahamu utamaduni wa jamii.
- Nitapania kuifahamu hadhira yangu pamoja na mahitaji yao.
- Nitatumia ufaraguni - uwezo wa kubadilisha sehemu fulani za sanaa bila kujifunga kwenye muundo asilia.
- Kumbukumbu nzuri - uwezo wa kukumbuka
- Nitabadilisha kiimbo kulingana na mahitaji.
- Kutumia viziada lugha k.v ishara za uso, ishara za mikono na miondoko mbali mbali n.k
- Nitaingenja taharuki kwa mtuo wa kidrama ili kuvuta nadhari ya hadhira yangu.
- Nitaishirikisha hadhira yangu kwa njia mbali mbali k.v uigizaji wa sehemu fulani, nyimbo n.k
- Nitaitumia lugha kwa uhodari ili kuipa mvuto.
- Nitavalia maleba yenye kuoana na nafasi ninayoigiza.
- Nitajenga mlahaka mwema na hadhira yangu.

**Zozote sita**

Tanbihi; mwanafunzi ajihusishe na majibu haya

Jinsi methali ni tanzu tegemezi

-  Hutumiwa mwishoni mwa ngano kufupisha maadili ya ngano
-  Hutumiwa kubuni lakabu za watu
-  Hutumiwa katika nyimbo na mashairi
-  Hutumiwa katika hotuba rasmi k.v mahakamani, dawaa
-  Hutumiwa katika kutoa funzo katika mawaidha
-  Hutumiwa katika tanzu za maadishi k.v riwaya, tamthilia n.k
-  Hutumiwa katika mazungumzo ya kawaida kuleta mvuto

**Zozote sita**